USAIDIZI WA KODI WA KAUNTI YA KING

UFADHILI HAUPATIKANI WA KUMSAIDIA KILA MPANGAJI MWENYE HITAJI.

KUSTAHIKI KWA MPANGAJI HAKUHAKIKISHI KWAMBA ATAPOKEA USAIDIZI .

Muhtasari wa Mpango:

Kaunti ya King itatumia njia mbalimbali za kuhudumia kwa haraka familia nyingi kama iwezekanavyo. Mpango wa usaidizi wa kodi utalipia baadhi ya majumba makubwa ya makazi ya makabaila na makao yaliyotengenezwa kwa kufanya malipo mengi kwa ajili ya wapangaji wanaostahiki. Kaunti hii itatafuta zaidi kusambaza msaada wa kodi ya wapangaji kwa makabaila wadogo ambao wapangaji wao wanaostahiki wanafaa usaidizi kupitia mchakato wa bahati nasibu. Ufadhili utapewa kipaumbele kwa maeneo yenye mahitaji mengi katika Kaunti ya King. Wiki tatu baada ya kuzindua kabisa mpango huu, Kaunti ya King itapitia familia zinazohudumiwa ili kuhakikisha mpango huu unatimiza mahitaji ya jumuiya na malengo na madhumuni ya mpango.

Kustahiki kwa Mpangaji: Lazima wapangaji watimize mahitaji yafuatayo ya kustahiki:

1. Mapato ni au chini ya asilimia 50 ya Mapato Wastani ya Eneo hili kwa siku 60 zilizopita; na
2. Angalau mwezi mmoja wa kodi haujalipwa au hujalipwa nusu tangu Machi 1, 2020.

Zaidi ya hayo, lazima wapangaji watimize MOJA au zaidi ya mahitaji yafuatayo.

1. Mzigo wa kodi: Asilimia 50 au zaidi ya mapato ya sasa ya kila mwezi inahitajika kulipia kodi.
2. Mpangaji awe hakuwa na makazi awali katika miaka mitano iliyopita; pamoja na uzoefu wa kutumia huduma za couch surfing/double up.
3. Historia ya kufukuzwa katika miaka saba iliyopita.
4. Makazi kutatizwa kwa sababu ya umbari, jamii, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kingono, au dini ya mwanafamilia.
5. Hatari ya ugonjwa sugu kulingana na CDC (miaka 62 au zaidi, hali zingine za kiafya).
6. Ulemavu wa mwanafamilia yeyote. Ikiwemo ulemavu wa kimwili, kukua, kiakili, au kihisia, pamoja na ulemavu unaosababishwa na pombe au matumizi ya dawa za kulevya, shida ya dhiki ya kiwewe, au upasuaji wa ubongo. Mtu aliye na HIV/UKIMWI huchukuliwa kuwa mlemavu.

Masharti ya Kabaila:
Kama masharti ya kupokea ufadhili, lazima makabaila wakubali:

1. Usaidizi wa kodi wa miezi mitatu kwa niaba ya mpangaji anayeshiriki kwa chini ya aidha: (a) asilimia 80 ya kodi ya jumla inayotumika kwa miezi mitatu; au (b) kodi inayolingana na hali ya soko kwa miezi mitatu. Deni lolote la kodi linalomilikiwa na mpangaji kwa zaidi ya miezi mitatu linapaswa kusamehewa. Ikiwa deni la kodi ni chini ya miezi mitatu, usaidizi unaweza kulipwa kwa kodi iliyopita na kodi ya baadaye hadi miezi mitatu lakini isizidi Desemba 2020.
2. Kutositisha au kukataa kubadilisha upya makubaliano ya upangaji ya mpangaji anayeshiriki hadi Machi 31, 2021.
3. Kutopandisha kodi kwa wapangaji wa sasa wanaohudumiwa na mpango huu hadi Machi 31, 2021.

Ikiwa mpangaji hastahiki na/au ikiwa kabaila hakubali masharti haya, familia hii haitahudumiwa.

Wapangaji Wanaotaka Usaidizi wa Kodi

Ikiwa unatimiza mahitaji ya kustahiki, tafadhali wasilisha nia yako kwa mpango wa Usaidizi wa Kodi wa Kaunti kwa kujaza fomu hii. **Haya si maombi**. Wapangaji watachaguliwa kwa bahati nasibu kila wiki. Bahati nasibu hii itazinduliwa Septemba 14, 2020. Ikiwa utachaguliwa katika bahati nasibu,shirika la jamii litawasiliana na wewe ambalo litakusaidia kukamilisha maombi haya.

Ikiwa hujachaguliwa katika bahati nasibu hii, utasalia katika kundi la wapangaji wanaotaka usaidizi na wanaostahiki kwa bahati nasibu zote zitakazofuata hadi fedha ziishe. Wapangaji ambao hawajachaguliwa watapokea barua pepe kila Ijumaa ***baada ya*** Septemba 14, 2020 ili kuwafahamisha kuhusu hali yao.

Ikiwa kabaila wako hatakubaliana na masharti haya ya kabaila, familia yako haitahudumiwa na mpango huu, hata kama unatimiza mahitaji ya kustahiki na umechaguliwa katika bahati nasibu.

USIJAZE FOMU ZAIDI YA MARA MOJA KWA KILA FAMILIA. Nafasi zako za kupokea usaidizi hazitaongezeka kupitia kuwasilisha mara kadhaa na zinaweza kucheleweshe muda wa kuchakata.

Una maswali? Mawasiliano: CommerceRAgrant@kingcounty.gov

Fomu ya Nia ya Mpangaji kutaka Usaidizi wa Kodi ya Kaunti ya King:

1. Je, familia yako inatimiza mahitaji ya kustahiki fedha hizi?
    - Ndiyo
    - Hapana

2. Unaishi katika Kaunti ya King? *Wakazi wa Kaunti ya King pekee ndio wanastahiki usaidizi huu. Ikiwa uko nje ya Kaunti ya King, tafadhali piga simu 211 au mamlaka ya eneo lako kwa usaidizi.*
    - Ndiyo
    - Hapana
3. Unaishi katika nyumba iliyotengenezwa/bustani ya RV?
    - Ndiyo
    - Hapana
4. Jina la Kwanza
5. Jina la Mwisho
6. Jina la Nyumba
7. Anwani ya Mtaa
8. Nambari ya Ghorofa (ikiwa hakuna, andika N/A)
9. Jiji
10. Msimbo wa Zip
11. Nambari ya Simu
12. Barua pepe *Tafadhali angalia mara mbili barua pepe yako kwa kuwa hii ndio itakuwa njia kuu ya kuwasiliana na wewe.*
13. Lugha yako unayopendelewa ni gani?
14. Unaweza kupokea huduma kwa Kiingereza?
    - Ndiyo

- Hapana

15. Jamii na kabila lako ni gani? Tafadhali weka tiki kwa zote zinazotumika
    - Mhindi Mwamerika / Mwalaska Asili
    - Mwasia / Mwamerika Mwasia
    - Mweusi / Mwafrika-Mwamerika / Mwafrika
    - Mwahawaii Asili / Mpasifiki wa Kisiwa
    - Mzungu
    - Mhispania / Mlatino
    - Jamii Nyingine Isioorodheshwa
    - Ninapendelea kutokusema
16. Uko katika kategoria gani ya umri?
    - Umri wa miaka 18-24
    - Umri wa miaka 25– 33
    - Umri wa miaka 34-54
    - Umri wa miaka 55+
17. Jinsia yako ni gani?
    - Mwanamke
    - Mwanaume
    - Sijitambui na jinsia yoyote
    - Nyingine

Ikiwa ulijibu Hapana kwa Swali 1-2, haustahiki ufadhili huu.

Ikiwa ulijibu Ndiyo kwa Swali 1-2, utawekwa katika kundi la bahati nasibu. Ukichaguliwa, shirika litawasiliana na wewe ili uwasilishe maombi. Uwasilishaji wa maombi hauhakikishi utapokea ufadhili.

Ikiwa hutachaguliwa katika bahati nasibu, utapokea barua pepe kila Ijumaa baada ya bahati nasibu kuzinduliwa mnamo Septemba 14, 2020 itakayokupasha kuhusu hali yako. Bahati nasibu itafanywa kila wiki.

Unapaswa tu kuwasilisha maombi yako mara moja, na utakuwa katika kundi la bahati nasibu kila wiki hadi fedha ziishe.

HAKUNA FEDHA ZA KUTOSHA ZA KUHUDUMIA KILA FAMILIA INAYOSTAHIKI.